

MARIA SPACES
12 OCT 2023
8PM
SAA 2 UCK

MAANDAMANO #KATIBAMPYA
#OKOABANDARIZETU , UMEJIPANGAJE KUSHIRIKI?

KATIBA MPYA

Space Title	MAANDAMANO #KATIBAMPYA #OKOABANDARI UMEJIPANGAJE KUSHIRIKI?
Space Date	12 OCTOBER 2023
Space Links	YouTube : https://www.youtube.com/live/8dSDhKcB38s?si=WOh_kNqykX_oEfma
	Twitter:
	ClubHouse:
	Facebook:

https://www.youtube.com/live/8dSDhKcB38s?si=WOh_kNqykX_oEfma

OVERVIEW

MWAMKO WA WANANCHI KATIKA KUPATA HARA KATI - TUNAPATAJE UMOJA WA KITAIFA?

#MariaSpaces #WenyeNchiWananchi #KatibaMpya #ChangeTanzania

Maandamano yameruhusiwa katika katiba yetu kama njia mojawapo ya wananchi kueleza na kutetea hoja zao kwa Serikali tawala. Watanzania wameamka na kuunganisha nguvu katika kutetea hoja zao kwa watawala kwa njia ya maandamano. Maandamano haya ya wananchi yamepangwa kuzinduliwa Mbeya tarehe 9 Novemba 2023. Katika hoja zitakazowasilishwa na wananchi ni kuupinga mkataba wa bandari ambao haujalenga kuleta manufaa kwa nchi bali kuwanufaisha waliopo madarakani. Hapo awali wananchi walitumia mahakama kuupinga mkataba huu lakini Serikali kwa mkono wake uliishinikiza mahakama kutoa hukumu iliyowapendelea. Ajenda ya pili itakayowakilishwa na wananchi katika maandamano haya ni takwa la wananchi kupata katiba mpya kabla ya uchaguzi wa 2025.

Haja ya katiuba mpya ni haja ya muda mrefu ya wananchi. Serikali imekua ikitumia mbinu mbalimbali kujihakikishia kuwa wanabaki madarakani kwa kuchelewesha mchakato wa kupata katiba mpya ili uchaguzi wa 2025 ufanyike bila ya katiba mpya. Takwa la wananchi ni kupata katiba mpya kabla ya uchaguzi wa 2025 ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unafanyika katika mazingira ya haki na usawa na tume huru ili serikali itakayopatikana iwe serikali ya wananchi itakayofanya kazi ya kuwatumikia wananchi. Ajenda ya tatu ya maandamano ya wananchi ni kuitaka serikali isitishe haraka kuhamisha wamasai kutoka kwenye maeneo yao ya asili ya Ngorongoro na Loliondo kwa kisingizio cha uhifadhi wakati imekua ikitoa ruhusa kwa wageni wa nje kuwinda na kujenga hoteli za kitalii.

Kufukuzwa kwa nguvu kwa Wamasai kumepelekea ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Hivyo wananchi wanaitaka Serikali itambue na kutimiza kwa haraka haki za Wamasai kwa ardhi ya mababu zao. Maandamano haya yataongozwa na Balozi Mstaafu Dk. Wilbrod Silaa, Mwanaharakati Mdude Nyangali, na Mwanasheria Boniface Mwabukusi. Maandamano yataendelea kufanyika tarehe 9 ya kila mwezi ila kupelekwa siku kadhaa mbele au nyuma pale ambapo tarehe hiyo itaangukia siku ya ibada (ijumaa, jumamosi au jumapili). Vazi la pamoja ni nguo/shati jeupe kuashiria kuwa ni maandamano ya amani.

Wananchi wamehimizana kuwa waangalifu kipindi cha maandamano hayo ili kujiepusha na makosa ya kisheria ambayo yanaweza kuzuia maandamano hayo lakini pia ili mapolisi wasiopate nafasi ya kuwakamata kwa makosa ya jinai. Vijana ndio nguvu kazi ya taifa na umoja wa wananchi ni wa muhimu katika kuleta mabadiliko kwani wasimamizi wa mwisho wa rasilimali zetu ni sisi wananchi.

#ChangeTanzania #WenyeNchiWananchi

ENGLISH VERSION

Demonstrations are legally allowed in our constitution as one of the ways for citizens to express and defend their arguments to the ruling Government. Tanzanians have woken up and joined

forces in defending their arguments to the rulers through protests. The citizens' public demonstrations are scheduled to be launched in Mbeya on November 9, 2023. The arguments to be presented by the public are to oppose the port agreement with DP World which is not aimed at benefiting the country but benefiting those in power. Previously, the people used the court to oppose this contract, but the Government with its hand pressured the court to give a verdict in their favor. The second agenda that will be represented by the people in this protest is the demand of the people to get a new constitution before the 2025 elections.

The need for a new constitution is a long-term need of the people but the government has been using various delaying tactics to ensure that they remain in power by delaying the process of obtaining a new constitution so that the 2025 elections can be held without a new constitution. The demand of the people is to get a new constitution before the 2025 elections to ensure that the elections are held in a fair and equitable environment with an independent commission so that the government that will be found will be a people's government that will work to serve the people.

The third agenda of the protests is to ask the government to immediately stop evacuating the Maasai from their ancestral lands of Ngorongoro and Loliondo under the pretext of conservation when it has been giving permission to foreigners to hunt and build tourist hotels in the same lands. The forced eviction of the Maasai has led to serious human rights violations. Therefore, the people want the Government to recognize and quickly fulfill the rights of the Maasai to their ancestral lands. This demonstration will be led by the former ambassador Dr. Wilbrod Silaa, activist Mdude Nyangali, and lawyer Boniface Mwabukusi. Demonstrations will continue to take place on the 9th of every month but will be moved several days ahead or behind when that date falls on a day of worship (Friday, Saturday or Sunday). The uniform for the protestors will be white dress indicating that it is indeed a peaceful protest.

Citizens have urged each other to be careful during the protest to avoid legal offenses that can prevent the protest but also so that the police do not get a chance to arrest any citizen for criminal offenses. The youth are the nation's workforce and citizens union is important in bringing about change as the ultimate say over the country's resources belongs to the citizens.

#ChangeTanzania #WenyeNchiWananchi